# MKATABA WA KUPANGISHA ARDHI KWA MRADI WA VIFAA VYA UJENZI

**KATI YA**

**ISACK DAVID MWAMBUNGU**

**(MPANGISHAJI)**

**NA**

**LYESI LIMITED**
**(WAPANGAJI)**

**KATIKA ARDHI ILIYOPO, KITALU 38B, ,MTAA WA MINAZINI**

**DAR ES SALAAM.**

**MKATABA WA KUPANGISHA ARDHI KWA MRADI WA VIFAA VYA UJENZI**

**MAKUBALIANO HAYA ya upangishaji** yamefikiwa leo, tarehe ..23.. Mwezi..OCTOBA..2024,

KATI YA

**ISACK DAVID MWAMBUNGU** wa S.L.P. 19980, Simu +255 769 664 182 Dar es Salaam, ambae katika mkataba huu atajulikana kama ("**Mpangishaji**") kwa upande mmoja

NA

**LYESI LIMITED,** ambayo ni Kampuni binafsi iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania kwa ajili ya kufanya shughuli za uzalishaji na usambazaji wa bidhaa za ujenzi na Masoko ya Dar es Salaam, Simu Nambari: +255 769 664 182 ambayo katika mkataba huu itajulikana kama (**Wapangaji"**) kwa upande mwingine.

KWA KUWA Wapangaji wana nia ya kupangisha eneo la ardhi tajwa lenye ukubwa wa **Sqm 2000** kwa ajili ya shughuli za uzalishaji wa vifaa vya ujenzi kwa malipo ya kodi na masharti Mengineyo yatakayoafikiwa kwenye mkataba huu;

**HIVYO BASI, MKATABA HUU ni uthibitisho wa makubalianao yafuatayo:**

1. KWAMBA Mkataba huu utaanza tarehe ya kusainiwa kwa mkataba huu na kuendelea kwa muda wa miaka minne tu (4) ukiwa na matarajio ya kuhuishwa ( renewal) kwa muda na kipindi kingine cha miaka minne kwa makubaliano ya pande zote mbili bila kuathiri kipengele cha kodi iliyokubaliwa katika mkataba huu.

2. KWAMBA Wapangaji watagharamia marekebisho yote watakayohitaji kufanya kuendana na shughuli zao za kilimo na mifugo.

3. KWAMBA Wapangaji wamekubaliana na mpangishaji kulipia gharama za kodi ya withholding tax

4. KWAMBA wapangishaji watakuwa na haki ya matumizi ya ardhi hiyo kama ifuatavyo:-

   **Mpangishaji :**

   (i) Atakua na haki ya kukusanya kodi ya kiasi cha Shilingi Laki TATU ( Tzs 300,000) kwa mwezi, kodi ambayo Wapangaji wanakubali kulipa kwa mkupuo mmoja kwa miezi sita yaani kiasi cha (Tzs 1,800,000) kwa miezi sita.

(ii) Atakua na haki ya kutembelea eneo husika kwa ukaguzi wa kawaida lakini kwa kutoa taarifa ya kimaandishi kwa njia yoyote rafiki na iliyokubaliwa na pande zote mbili kama vile, barua pepe, barua au ujumbe mfupi wa simu siku 3 kabla ya siku iliyokusudiwa.

**B. Wapangaji:**

(i) Sehemu ya ardhi mita za mraba (sqm 2000) itakodishwa kwao kwa kipindi cha muda na kodi iliokubaliwa katika mkataba huu.

(ii) Haki ya kutobadilishiwa kiwango cha kodi kwa muda wote wa upangaji kama ilivyokubaliwa katika mkataba huu.

(iii) Haki ya kukaa na kufanya shughuli zao za biashara za kampuni bila bughudha zozote kutoka kwa wapagishaji au wahusika wowote kwa upande wake ikiwa katika muda wote wapangaji wamezingatia masharti ya upangaji kama ilivyoainishwa katika mkataba huu ikiwa ni pamoja na kulipa kodi kama ilivyokubaliwa.

5. KWAMBA Mpangishaji na Wapangaji watashirikiana katika kutunza mazingira na kulipa ankara za madai ya umeme na maji kwa kipindi chote cha uhai wa mkataba huu.

6. KWAMBA, sehemu ya ardhi hii imepangishwa ikiwa pamoja na vyote vilivyomo ndani ya ardhi husika ambavyo Wapangaji watakua na haki ya kuvitumia.

7. KWAMBA, Wapangaji endapo watahama basi watalazimika kuacha ardhi katika hali ya usafi na kulipa ankara zote zenye malimbikizo ikiwamo ya umeme na maji.

8. KWAMBA, Wapangaji watatakiwa kutoa taarifa ya maadishi ya kuendelea ama kusitisha mkataba mwezi mmoja kabla ya mkataba huu kumalizika.

9. KWAMBA Wapangaji na Mpangishaji wanaweza kusitisha mkataba huu kwa kutoa taarifa kwa maandishi mwezi mmoja kabla ya kukatisha mkataba huu na taarifa zozote kuhusu mkataba huu zitahesabika kuwa zimetolewa ikiwa zitatumwa au kufikishwa moja kwa moja kwa wahusika na katika anuani zifuatazo;

Wapangaji,
Lyesi Limited,
S.L.P. 19980
Dar es Salaam.
Mob: +255 769 664 182

10. KWAMBA iwapo pande husika zitahitilafiana kuhusu tafsiri au utekelezaji wa vipengele vya mkataba huu, basi mgogoro huo utatatuliwa kwa njia ya majadiliano na endapo hakutakua na suluhu ya mgogoro huo basi upande usio ridhika utakua na nafasi ya kufungua shauri katika mahakama husika ili kupata nafuu stahiki.

11. KWAMBA, Mkataba huu umefungwa na kusimamiwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**KWA UTHIBITISHO wa makubaliano haya, wahusika wameweka saini zao katika hati hii kama inavyoonekana hapa chini:**

IMEWEKWA SAINI jijini Dar es Salaam na }
**NA ISACK DAVID MWAMBUNGU.** } ..............................
ambaye ninamfahamu, leo tarehe ...23... }
mwezi wa ...October... 2024. }

SAINI: ..............................
JINA: Pius Alphonce Musiba
TAREHE: 23/10/2024
WADHIFA: Wakili

Pius Alphonce Musiba
P.O.Box 19980 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

IMEWEKWA SAINI na Lakiri/Muhuri jijini Dar es Salaam na }
**Kwa niaba ya Lyesi Ltd** }
ambaye ninamfahamu, leo tarehe ...23... }
mwezi wa ...October... 2024. }

..............................
**Muhuri/lakiri**

LYESI LIMITED
P.O. Box 19980
DAR ES SALAAM

SAINI: ..............................
ANWANI: 19980 DSM
TAREHE: 23/10/2024
WADHIFA: Mkurugenzi.

SAINI: ..............................
ANWANI: 19980 DSM
TAREHE: 23/10/2024
WADHIFA: Mkurugenzi.